


# ZAIDI YA SHILINGI BIL. 100 ZIMETENGWA KWAAJILI YA HUDUMA ZA CHANJO

Na Hassan Kimweri - Dodoma



Katika kuimarisha huduma za Kinga dhidi ya magonjwa kiasi cha zaidi ya shilingi Billioni Mia Moja (Bil. 100) zimetengwa kwaajili ya kutoa huduma za chanjo kwa watoto nchini.

Waziri wa afya Mhe. Ummy Mwalimu ameyasema hayo Mei 12, 2023 wakati akiwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara ya afya kwa mwaka 2023/24 kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Fedha hizi zitaenda kununua, kutunza na kusambaza chanjo kwa gharama ya Shilingi Mil. 87,044,538,781, kununua majokofu 1,601 ya mnyororo baridi wa chanjo yenye thamani ya Shilingi 21,025,327,723, kununua magari 102 ya kusambazia chanjo yenye thamani ya Shilingi 6,299,372,400." Amesema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy amesema hadi kufikia mwezi Machi 2023 jumla ya watoto 1,596,951 sawa na 98.6% walikuwa wamechanjwa chanjo ya Penta3 kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya Dondakoo, Kifaduro, Kupooza, homa ya ini na homa ya uti wa mgongo ambayo hutumika kama kipimo kikuu cha chanjo ikilinganishwa na 94.6% mwaka 2021/22.

"Jumla ya Wasichana Laki Tano na Elfu Thelathini na Tano Mia Saba na Nane (535,708) wenye umri wa miaka 14 wamepatiwa chanjo ya kuzuia Saratani ya mlango wa kizazi (HPV)." Amesema Waziri Ummy

**MAGARI 102**
ya kusambaza chanjo kununuliwa

# MATUKIO KWENYE PICHA, UWASILISHAJI WA BAJETI YA WIZARA YA AFYA BUNGENI MEI 12 & 15 2023.



Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu, akiwasilisha Hotuba ya Bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/24 Bungeni Jijini Dodoma.



Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu, akiteta jambo na Naibu Waziri wa Afya Mhe. Dkt. Godwin Mollel mara baada ya kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/24 Bungeni Jijini Dodoma.



Timu ya madaktari bingwa 100 wa masuala ya afya ya uzazi, mama na mtoto ambao ni wageni waalikwa wa Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu wakifuatilia uwasilishwaji wa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2023/24.



Viongozi wakuu wa Taasisi za Wizara ya Afya wakifuatilia uwasilishwaji wa hotuba ya bajerti ya Wizara ya Afya Bungeni.



Watumishi kutoka Wizara ya Afya wakifuatilia uwasilishwaji wa hotuba ya bajerti ya Wizara ya Afya Bungeni.

